

# SwahiliWeb

ELECTRONIC DEPOSITORY AND RESOURCE ARCHIVE

[www.swahiliweb.net](http://www.swahiliweb.net)

Archive: Pat Caplan

Document: Ngwari Malim and his wife

File reference: SW/PC/I3017

This document has been downloaded from the SwahiliWeb archive on the understanding that it is copyright under the laws of the United Kingdom and the Berne Convention, and that no further copying, storage or distribution, in any form or by any means, including electronically, is permitted except under the provisions of fair dealing.

Copyright of all materials deposited with SwahiliWeb remains with the copyright holder. Those seeking copyright and associated permissions will be referred to the copyright holder.

**Interview with Ngwari Malim and his wife, 1985,  
transcribed by Joseph Bwaithondi 2011**

*Ngwari was the younger half brother of my adopted 'older brother' and thus also my 'brother', although my relationship with him was not as close as that with his older brother. At the time of this interview, I estimate that the couple were in their forties.*

**Topic: What is better? Men's or women's lives?**

PC: Mama unaonaje, bora maisha ya mwanamke au ya mwaname hapa Mafia?

Ngwari: Mimi naomba hapo kusema maisha gani ya kuishi na Ngwariamme au kuolewa au ya kutoolewa

PC: Yaani kama Mungu angekuuliza kama ukizaliwa tena ungependa kuzaliwa kama mwanaume au mwanamke?

Ngwari: Kitu gani kingeweza kukusaidia kuishi kama mwanamme au mwanamke

Wife: Mie ningependa kuzaliwa kama mwanamme

PC: Kwa nini?

Wife: Ana maharifa mengi.

PC: Wewe

Ngwari: Mie ukiniuliza nitaelekea huko huko kwa mwanamme

PC: Sawa.

Neighbour: Haya kwe herini Si utapita nyumbani

PC: Ndio

**Sex preferences for children**

PC: Na katika kupata watoto utapenda mtoto wa kiume au wa kike?

wife: Bora wa kiume.

PC: Sababu.

Wif: Sababu sie watoto wakike tukiwa peke yetu tukiwafata wale watoto wa kiume wanatusaidia.

PC: Wewe unasemaje?

Ngwari: Mimi nikizidi kupanua mawazo mtoto wa kike akiolewa anakwenda huko , wakati wa kiume yeye ataweza kukujengea

Wife: Hata kama kweupe ataweza kukujengea ila wa kike kazi yake ni kukuchotea maji kukufulia kukupikia sawa.

*Is life better now or before?*

PC: Ukitizama hali ya maisha hapa Mafia na ukitizama hali ya maisha miaka 20 iliyopita bora ipi? Sasa ua siku za nyuma?

Wife: Bora siku za nyuma

PC: Sababu

Wife: Siku za nyuma, siku hizi kuna matatizo

PC: Matatizo gani?

Wife: Siku hizi hali ni magumu.

PC: Kivipi?

Wife: Matatizo

PC: Matatizo yepi?

Wife: Mengi sana. Kuna shida nyingi

PC: Yako mwenyewe

Wife: Hata ya ulimwengu mzima. ZaNgwarii na sasa mbalimbali

PC: Unaweza kunieleza zaidi?

Wife: Sasa kuna vitu ghali na hatuvioni, ZaNgwarii ulikuwa unaviona na havikuwa ghali.

Ngwari: Karibu machungwa mama

PC: Ahsante nimeshakula sana.

*Who works harder – men or women?*

PC: Katika jamii ya hapa Mafia ni nani anafanya kazi sana mwanamke au mwanamme

Wife: Kazi zaidi, huo mtihani, ukienda huku mazito na ukirudi huku mazito lakini wanawake wanafanya zaidi

PC: Wewe unasemaje

Ngwari: kuhusu nini?

PC: Katika Mafia hii nani kati ya mwanamke na mwanamke anafanya kazi zaidi?

Ngwari: Katika kufanya kazi. Pendekezo langu naona ni mwanamme.

PC: Sababu?

Ngwari: kwa sababu anafanya kazi zote. Kazi ya kwanza ende akalime unasikia, haje akatafute chakula, nazi akamletea mwanamke unasikia , kitoweo unasikia, kiungo unasikia, sukari unasikia na kasha akamletea mwanamke ili akae kitako akapike chakula, anatafuta vitu vya kukamilisha nyumba mzima. Pande zingine hata kuni na maji akamlatee mke. Mama naomba unisubiri kidogo Ngwarieno yako mazuri namuondoa huyu bwana ana njaa.

PC: Mama hii ndio harusi yako ya kwanza?

Wife: Na mume huyu?

PC: Ndio

Wife: Ehe!

PC: Ukuwahi kuolewa

Wife: Hapana.

*Her children*

PC: Watoto umezaa nae wangapi

Wife: Wangu mie kumi ila watatu hawapo tena

PC: Wajinsia gani waliopote?

Wife: Mmoja wa kiume na wawili wa kike.

PC: Walikuwa na umri gani?

Wife: Mmoja hakuona duniani (alikuwa akiwa tumboni baada ya miezi tisa) mmoja wa kiume alipita tu na mwingine alikaa kitako kidogo.

PC: Mmoja mwanamke hakuja na roho, na mwingine wa kike

Wife: hakuja na roho vilevile

PC: Katika waliobaki wakike wangapi na kiume wangapi?

Wife: Mmoja wa kike na waliobaki ni wakiume.

PC: Ina maana waliobaki saba

Wife: Saba?? Ngoja tuwahesabu: Omari ,Riziki, Hamisi,Hamidi na huyu na dada yao

PC: Kwa hiyi ni sita ?

Wife: Ndio.

PC: Na wanawake waliopotea ni watatu.

Wife: Hawa wawili hawakuja kabisa ila huyu mmoja alikuja na akakaa kama miezi minne mitano hivi.

PC: Tuseme katika kuzaa watoto tuseme watoto wangapi ni wazuri. Ni nzuri kuzaa watoto wengi wengi au kuzaa watoto kama wachache

Wife: Kuzaa kama wengi?

PC: Mmh!

Wife: Kuzaa wachache.

PC: Kama engeweza kuchagua kuzaa watoto ungependa kuzaa watoto wangapi

Wife: Kama kuchagu wanaume na wanawake sio sawa.

PC: Binti yako kaolewa wapi?

Wife: Kaolewa Bweni.

PC: Lakini anakuja kukutazama

Wife: Ndio

PC: Ameshapata watoto?

Wife: Bado

PC: Imekuwa bahati mbaya bado hajapata mtoto

*Women describes her daily routine*

PC: Sasa kutoka asubuhi unapoamka mpaka jioni unapoenda kulala unafanya nini? Kazi gani?

Mwanamke: Naamka nakaa nyumbani kwangu tu nafagia napika nachota maji

PC: Maji unachota wapi?

Wife: Huko bondeni kwa Salum Nassoro

PC: Mbali?

Wife: Hata si mbali, Wewe si ulikwenda siku ile?

PC: Si mbali. Na wewe katika siku moja unatumia ndoo ngapi?

Wife: Ndoo mbili tatu basi.

PC: Halafu kupika. Unapika chai tu au?

Wife: Napika na chakula kingine kama ninacho. Napika kama muhogo ndizi.  
Mchana vile vile napika

PC: Baada ya chai unafanya kazi gani?

Wife: Nakwenda kulima

PC: Halafu mchana unapika tena?

Wife: Napika

PC: Halafu

Wife: Nakwenda kuvuna kama kuna kuvuna mpunga.

PC: Lini unakwenda kutafuta kuni?

Wife: Kuni?

PC: Unakwenda kila siku kutafuta kuni?

Wife: Nakwenda siku moja moja ,nakwenda kila baada ya siku tatu ya nne  
nakwenda kutafuta kuni.

PC: Muda gani unakwenda asubuhi au mchana au jioni?

Wife: Muda wowote ule.

PC: Kutwanga

Wife: Natwanga

PC: Unatwanga mwenyewe?

Wife: Ninamsaidizi hapa

PC: Unatwanga mara ngapi kwa siku?

Wife: Mara moja

PC: Muda gani?

Wife: Hasa jioni.

PC: Kuosha viombo?

Wife: Naosha mwenyewe

PC: Huna mtoto wa kike .

Wife: Ndio

PC: Sasa unapumzika lini?

Wife: (Kicheko) Mapumziko yenyewe ni muda wa kulala. Kama saa tatu au nne au tano

PC: Akhsante sana.

PC: Sasa nitamuuliza bwana. Toka asubuhi unapoamaka mpaka jioni unapoenda kulala unafanya nini?

Ngwari: Toka asubuhi mpaka wakati wa kulala. Mimi nafanya kazi tatu kwa tano .

PC: Niuambie kwanza

*Ngwari describes his routine*

Ngwari: Kwanza nikiamka natia mswaki na kunawa uso pamoja, nakunjwa chai, nafuta vyombo halafu nakwenda kazini kukata tuta moja la viazi. Halafu nashika mundu nakwenda kwenye minazi palepale Mundu naunga kidogo pale. Kuunga unajua?

PC: Hapana.

Ngwari: Kuondoa yale makoko kama hivi kwenye minazi halafu napanda mihogo na miche ya midizi unasikia? Ngapi hiyo?

PC: Tatu

PC: Kazi hizo za kulima unazifanya kwa muda gani? Toka saa ngapi mpaka saa ngapi

Ngwari: Kazi hizo naanza kuzifanya toka muda wa saa mbili mpaka kwenye saa sita kisha narudi nyumbani kupumzika na kula.

PC: Ukishakula na kuumzika unafanyua nini

Ngwari: Nakwenda kwa vijana wenzangu kucheza karata, bao halafu narudi nyumbani

PC: Kama saa ngapi?

Ngwari: Kama saa kumi na mbili.

PC: Chakula cha jioni unakula saa ngapi?

Ngwari: Huku kwetu hakuna muda maalum kuna wakati saa moja mara moja unusu Hakuna muda mahalum.

PC: Ukishakula unafanya nini?

Ngwari: Nalala

PC: Kama saa ngapi?

Ngwari: Kama saa mbili au tatu Ngwariake nikishakula nasikiliza redio halafu nalala. Uliza jingine

PC: Mbona mtihani.

Ngwari: Mie napenda uniulize.

*How much of their food do they grow themselves?*

PC: Katika chakula unacholima kintasha mwaka mzima au unanuna kingine?

Ngwari: Kuna wakati sinunu hata cha senti tano, nalima mpunga, viazi vitunguu. Lakini kuna wakati mwenyezi Mungu anakutendea inabidi unanunua

PC: Sababu

Ngwari: Kuna wakati kuna jua kali haupati kitu au mvua nyingi mpunga unazama

PC: Chakula kinacholimwa hapa ni mpunga tu??

Ngwari: Nimekwambia chakula kinacholimwa hapa sio mpunga tu , tuna mihogo, vianzi ndizi hata Ngwarianasi tunapanda

PC: Sasa wewe unakula mpunga kila siku?

Ngwari: Mimi? Hapana siku nyingine nakula viazi jioni siku nyingine muhogo jioni. Nabadili. Wewe huliza tu yote.

*What food is good for children?*

PC: Katika Kulea watoto chakula gani kizuri?

Ngwari: Katika kulea watoto kwetu zama za mababa zetu ubwabwa wanachanganya na mtindi ndio unalishwa.

PC: Mtoto wa umri gani anaanza kulishwa hiki chakula?

Ngwari: Wengine miezi mitatu mpaka unatambua mambo. Ila kwa watoto wangu hawa nimeanza kuwalisha baada ya miezi sita. Chakula chao maziwa ya mama yao na ya n'gombe. Wakishafika miezi sita ndio naanza kuwapatia uji kidogo kidogo. Mpaka tena kutambua mwenyewe.

PC: Kuna chakula chochote ambacho hakifai kumpa mtoto?



Ngwari: Kuna vyakula ambayo ukiwapatia watoto wanakuwa hawana sura barabara. Kama huo ubwabwa. Kuna watoto wengine unawasumbua

*Who needs more food?*

PC: Baina ya wanawake na wanaume nani anahitaji chakula zaidi?

Ngwari: Oni langu mie mwanamme anahitaji chakula haraka kuliko mwanamke. Mwanamke anastahimili njaa na mwamme hastahimili njaa. Hata mtoto wa kike anastahimili njaa kuliko wa kiume.

PC: Hivyo

PC: Katika nyumba yako wakati wa kula chakula, je mnakula pamoja au wanawake wanakula kwa upande mmoja na wawake kwa upande mwingine?

Ngwari: Sawa. Nyumbani kwangu mimi kwa kawaida kama nafikwa na wageni tunakula mbali mbali lakini kama tupo sisi tu tunakula pamoja. Uliza jingine na uchague zito.

*How did you get your coconut trees?*

PC: Sasa nakuuliza kuhusu shamba lako je ulilipata vipi? Ulirithi au ulivunja pori au minazi?

Ngwari: Nilirithi, nilivunja pori kwa mikono yangu na bibi

PC: Panaitwaje

Ngwari: Kipanje.

PC: Hapa je hapakuwa na minazi?

Ngwari: Hapa nimerithi na kulikuwa na minazi

PC: Kipanje?

Ngwari: hapo tumevunja pori na bibi na kupata midizi na mihogo ila mihogo imekauka kutokana na jua kali

*Did you use immigrant labour?*

PC: Je mmewahi kutumia wageni katika kilimo?

Ngwari: Tumewahi katika shamba la Kipanje. Kama kupiga matuta

PC: Umewatumia kwa muda gani?

Ngwari: Toka mwaka jana. Niwatumia Wamakonde, Jamaa wa kinyamwezi

PC: Kazi hiyo hiyo ya kupisha matuta?

Ngwari: Kupigisha matuta na kufyeka miti

PC: kutoa visiki

Ngwari: Sikutoa

PC: Kujenga koti?

Ngwari: Najenga mwenyewe

PC: Kupanda

Ngwari: Napanda mwenyewe na watoto wetu

PC: Kupalilia

Ngwari: Watoto wetu.

*Have you ever used big hoes? Yes he has*

PC: Katika kulima wewe umewahi kutumia jembe kubwa au wewe umetumia majembe madogo madogo?

Ngwari: Katika kulima natumia jembe kubwa linaitwa kablini

PC: Katika kulima ni mwanamke naye analitumia hili jembe?

Ngwari: Mwanamke pia anaweza kulitumia

Ngwari( Anamuonyesha hilo jembe)

PC: Hili sio kubwa sana?

Ngwari: Hili limekwisha ndio maana na linatumika katika kupalilia na sio kulimia.

PC: Je unatumia jembe ili katika kupanda

Ngwari: Hapana natumia jembe lile dogo

PC: Mama unalo shamba lako mwenyewe la kulima

Ngwari: Hana.

Wife: Sina tunalima pamoja

Ngwari: Hata na mimi sina tunalima shamba pamoja.

PC: Mie nimemaliza sasa kama mnaweza kuondoka mnaweza.

*Why do some men like to marry more than one wife?*

PC: Napenda kukuuliza hivi kwa nini wanaume wengine wanape kuo  
wanawake watatu mpaka wawili?

Kicheko.

Ngwari: kutafuta ni kote pande mbili unasikia. Kama nimelima shamba  
kubwa ninabidi niwe na mji zaidi ya mmoja ili tuweze kulihifadhi. Maana ya  
pili kama nikiowa halafu sikupata mtoto itabidi niowe mwingine ili kizazi  
kisipotee.

PC: Je mama unasemaje kuhusu ili?

Wife: Sijuhi

PC: Je wewe ungelipenda kuolewa na wanaume wawili

Wife: Ningependa kuolewa hivyo

Kicheko.

Wht re the main problems on Mafia

PC: Katika hapa Mafia matatizo makubwa hapa ni nini?

Ngwari: Ngoja kwanza

Wife: Matumizi hakuna ya vitu mbali mbali kama viombo na kadhalika.

PC: Wewe unasemaje

Ngwari: Mimi sipendi kumzunguka ila moja..... **the end of the tape**